Australian Red Cross

Get Prepared - Swahili



# Dharura hutokea.

Habari njema ni, kuna mambo rahisi unayoweza fanya kujiandaa.



**Liwe ni Janga la asili, ajali ya gari au janga la ulimwengu, dharura huleta changamoto kubwa dhidi ya kusababisha athari mbaya maishani mwetu.**

Jiandae kimawazo, fikiria jinisi unavyo weza kujitayarisha ili kupambana na dharura wakati wa shida. Na ukijipata katika pilka pilka za dharura jaribu kuwa mtulivu. Hii itakusaidia kufanya uamuzi dhabiti.

## Pata Kujua

Jifunze jinisi unaweza kabiliana na adhari kupitia rasilimali kama Msalaba mwekundu, Maktaba, huduma za dharura au watu ambao wameishi katika eneo lako kwa muda mrefu.

## Unganika

Kwa kujiunga na watu katika jamii, inamaanisha mnaweza kusaidiana wakati wa dharura. Kueneza mtandao wako, unaweza kujiunga na klabu, kujitolea katika shirika ama kujulia jirani yako hali na kuwa na anwani yake kwa minajili ya mawasiliano.

## Jipange

Fikiria jinsi unaweza jitayarisha iwapo kuna dharura. Kwa mfano, toa nakala za Stakabadhi muhimu na uziweke asilia mahali pema. Ni vyema kujua na kulinda vitu vya hisia na thamani. Pia ni wazo zuri kujipanga dhidi ya dharura na kupakia mfuko wa dhiki utakapohitajika kuondoka haraka nyumbani mwako. Dharura hutokea, ni vyema kuwa umejiandaa.

Ili kujifunza zaidi, tembelea tovuti la Msalaba Mwekundu Australia au pakua Programu ya kujitayarisha ya Msalaba Mwekundu.

Australian Red Cross

GET PREPARED
Protect what matters most
Download on the App Store
Android app on Google play

SWAHILI